Watu nje ya Amerika: Maafikiano haya yanaweza kukuathiri kwa sababu yanashughulikia hisa ya hakimiliki ya Amerika katika vitabu vilivyochapishwa nje ya Amerika. Kama una hisa katika kitabu au nyenzo zingine katika kitabu, maafikiano haya yatakufunga isipokuwa uamue kutoshiriki kwa wakati unaofaa.

Kama wewe ni Mwandishi wa Kitabu, Mchapishaji Kitabu au Mtu Mwingine Anayemiliki Hakimiliki ya Kitabu Au Maandishi Mengine,

Haki zako zinaweza kuathiriwa na maafikiano ya hatua ya pamoja kuhusiana na uchanganuaji wa Google na utumiaji wa Vitabu na maandishi mengine.

Waandishi na wachapishaji waliwasilisha kesi ya hatua ya kitengo, wakidai Google ilikiuka hakimiliki za waandishi, wachapishaji na wamiliki wengine wa hakimiliki ("Wamiliki haki") kwa kuchanganua katika Vitabu na Vipachiko vyenye hakimiliki na kuonyesha madondoo bila ruhusa. Google imekataa madai haya. Vyama hivi vimekubali maafikiano. Muhtasari huu unatoa taarifa msingi kuhusu maafikiano. "Vitabu" na "Vipachiko" vimefafanuliwa hapa chini.

Je, Maafikiano haya Yanatoa nini?

Maafikiano haya, kama Korti itaidhinisha, yataruhusu Google kuchanganua katika Vitabu na Vipachiko vyenye hakimiliki nchini Amerika, na kutunza hifadhidata ya kielektroniki ya Vitabu hivyo. Kwa vitabu ambavyo vimeachwa kuchapishwa na, kama imeruhusiwa na Wamiliki haki wa Vitabu vinavyoendelea kuchapishwa, Google itaweza kuuza ufikiaji wa Vitabu hivyo na taasisi kujiandikisha kwa hifadhidata hiyo, kuweka matangazo kwenye ukurasa wowote wa Kitabu, na kutumia Vitabu hivyo kwa matumizi mengine ya kibiashara. Wakati wowote ule, Wamiliki haki wanaweza kubadilisha maagizo ya Google kuhusu matumizi haya. Kupitia Rajisi ya Haki za Vitabu ("Rajisi") ilioanzishwa na maafikiano hayo, Google itawalipa Wamiliki haki asilimia 63% ya mapato yote kutoka kwa matumizi haya.

Google pia italipa $ milioni 34.5 ili kuanzisha na kufadhili operesheni za kwanza za Rajisi na gharama za kusimamia ilani na maafikiano kwa kulipa pesa taslimu $ milioni 45 kwa Wamiliki haki wa Vitabu na Vipachiko ambavyo Google huchanganua kabla ya siku ya mwisho ya kuamua kutoshiriki katika maafikiano hayo.

Je, ni nani aliyejumuishwa?

Kitengo cha Maafikiano kinajumuisha watu wote ulimwenguni kote ambao wanamiliki hisa ya hakimiliki ya Amerika katika Kitabu au Kipachiko chochote. **Maana ya "Hisa ya hakimiliki ya Amerika" ni pana. Mahali popote ulipo, tafadhali soma Ilani kamili ili uamue kama umejumuishwa katika maafikiano haya.**

Kuna Vitengo viwili vidogo:

- *"Kitengo Kidogo cha Waandishi"* (waandishi wa Vitabu na maandishi mengine, na warithi, wandamizi na waawaza wao), na
- "*Kitengo Kidogo cha Wachapishaji"* (wachapishaji wa Vitabu na mapambizo, na warithi na waawaza wao).

Je, ni Vitu Gani Vilivyoshughulikiwa?

"Vitabu" vinajumuisha kazi ilioandikwa yenye hakimiliki, kama vile riwaya, vitabu vya maandishi, tasnifu, na maandishi mengine ambayo yalichapishwa au kusambazwa katika muundo wa nakala ngumu kabla ya tarehe **5 Januari 2009**. Kazi za Amerika lazima zisajiliwe na Ofisi ya Hakimiliki ya Amerika ili zijumuishwe katika maafikiano. "Vitabu" havijumuishi mapambizo, makaratasi ya kibinafsi, karatasi ya muziki, na kazi ya umma au serikali.

"Vipachiko" hujumuisha maandishi yoyote na vitu vingine, kama vile barua za kusambazwa, insha, mashairi, nukuu, barua, maandishi ya wimbo, maonyesho ya Vitabu vya Watoto, karatasi ya muziki, chati, na grafu, kama imelindwa kivyake na hakimiliki ya Amerika, iliojumuishwa katika Kitabu, kazi ya serikali au kitabu cha umma kilichochapishwa kabla ya tarehe **5 Januari 2009** na kama ni Kazi ya Amerika, iliosajiliwa na Ofisi ya Hakimiliki ya Amerika (ikiwa kivyake au kama sehemu ya kazi nyingine). Vipachiko havijumuishi yaliyomo kwenye picha (isipokuwa kwa maonyesho ya Vitabu vya Watoto), au kazi yoyote ya umma au ya serikali.

Ilani hii inajumuisha ufafanuzi zaidi wa kina wa masharti haya na taarifa zingine muhimu kuhusu maafikiano haya.

Je! Nifanye nini?

Tafadhali soma Ilani kamili, ambayo inapatikana kwenye http://www.googlebooksettlement.com. Amua kama aidha:

- Utabaki katika maafikiano. Ukifanya hivyo, utafungwa na maamuzi ya Korti, pamoja na kuachilia madai yako dhidi ya Google.
- Utapinga au au kutoa maoni juu ya maafikiano. Lazima upinge/utoe maoni kwa kuandika kabla ya tarehe **5 Mei, 2009.**
- Utaamua kutoshiriki katika maafikiano na utunze haki yako ya kushtaki Google kivyako. Lazima uamue kutoshiriki kwa kuandika kabla ya tarehe **5 Mei, 2009.**
- Utawasilishe madai ya malipo ya pesa taslimu (kama unastahiki kufanya hivyo). Lazima uwasilishe madai yako kabla ya tarehe **5 Januari 2010.**

Korti imemteua Mshauri wa Kitengo ili kuwakilisha Vitengo hivi viwili vidogo. Kama maafikiano yataidhinishwa, Mshauri wa Kitengo wa Kitengo Kidogo cha Waandishi ataomba ada ya wakili na gharama ambazo Google imekubali kulipa. Unaweza pia kuajiri wakili wako mwenyewe kwa gharama yako mwenyewe.

Korti itaamua kama itaidhinisha maafikiano katika Usikilizaji usio na upendeleo mnamo **tarehe 11 Juni 2009, saa saba mchana.**

Pata maelezo kamili, pamoja na Ilani Kamili:

Tembelea: http://www.googlebooksettlement.com Call: 000 1.612.359.8600

Write: Google Book Search Settlement Administrator, c/o Rust Consulting
P.O. Box 9364, Minneapolis, MN 55440-9364 UNITED STATES OF AMERICA